JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**Kumb. Na. EB.32/160/01/207** **28 Februari, 2025**

Afisa Mtendaji Mkuu,
Green Star Media Limited,
T/A Key FM,
S.L. P 1666,
**57117 SONGEA.**

# UAMUZI JUU YA AMRI YA UTEKELEZAJI

*(Kwa mujibu wa Amri ya Utekelezaji iliyotolewa kwa Green Star Media Limited tarehe 10 Januari, 2025)*

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (inayorejewa kama **"Mamlaka"**) mnamo tarehe 14 Oktoba 2021, ilitoa leseni ya Huduma za Utangazaji kwa njia ya Redio (inayorejewa kama "**Leseni")** pamoja na rasilimali ya Masafa ya Redio kwa kampuni ya Sibuka FM Limited t/a Key FM (inayorejewa kama "**Mtoa Huduma**") kwa ajili ya utoaji wa huduma za utangazaji.

1.2 Kampuni ya Green Star Media Limited wakati inapewa leseni na Mamlaka ilikuwa na wanahisa watatu ambao ni:

(a) Castory Carlos Ndullu aliyekuwa akimiliki jumla ya hisa 1100;

(b) Joyce John Mashimba aliyekua akimilika jumla ya hisa 200; na

(c) Ndulu Group of Companies Limited aliyekua akimiliki jumla ya hisa 100.

1.3 Leseni iliyotolewa kwa Mtoa Huduma ilimtaka Mtoa Huduma, katika kutoa huduma zinazosimamiwa na Mamlaka, kufuata sheria, kanuni, masharti ya leseni na maelekezo ya Mamlaka yanayotolewa mara kwa mara.

1.4 Kanuni ya 23(1) ya Kanuni ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018, inamtaka mleta maombi ya leseni au mtoa huduma kutofanya mabadiliko katika muundo wa umiliki wa hisa bila idhini ya Mamlaka.

1.5 Kanuni ya 23 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni za Mwaka 2018 inamtaka mtoa huduma za utangazaji kuhakikisha angalau asilimia mbili (2%) ya maudhui yake ya siku yanahusu elimu.

1.6 Kanuni ya 39(4)(a) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni za Mwaka 2018 inamtaka mtoa huduma za utangazaji kuhakikisha anawasilisha kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ratiba yake ya vipindi siku kumi na nne (14) kabla ya robo ya mwaka kuanza.

1.7 Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake ya kiudhibiti, ilifanya uchunguzi na kubaini kuwa Mtoa Huduma: -

a) amebadilisha umiliki na muundo wa hisa kutoka umiliki wa awali aliowasilisha wakati akiomba Leseni kwenda kwa wamiliki wengine ambao kwa mujibu wa taarifa za Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umiliki wa hisa wa kampuni ya Mtoa Hudumani ni kama ifuatavyo:
   (i) Boniface Godwin Mwamposa anamiliki hisa1600;
   (ii) Castory Carlos Ndulu anaye miliki hisa 10;
   (iii) Blessing Macklin Mwaitenda anayemiliki hisa100;
   (iv) Jackson Whatson anayemiliki hisa 100; na
   (v) Immanuel Titus Sanga anayemiliki hisa 100

b) Ameshindwa kuhakikisha angalau asilimia mbili (2%) ya maudhui yake ya siku yanahusu elimu; na

c) Ameshindwa kuhakikisha anawasilisha kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ratiba yake ya vipindi siku kumi na nne (14) kabla ya robo ya mwaka kuanza.

2.0. **AMRI YA UTEKELEZAJI**

Mnamo tarehe 10 Januari 2025, Mamlaka ilitoa Amri ya Utekelezaji kwa Mtoa Huduma, ikimtaka kuwasilisha utetezi wake kimaandishi na kufika katika ofisi za TCRA Makao Makuu Dar es Salaam tarehe 24 Januari 2025, saa tano (5:00) asubuhi kujieleza kwa nini asichukuliwe hatua za kisheria kwa:

(a) kubadili umiliki wa hisa pasipo idhini ya Mamlaka kinyume na Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018.

(b) kushindwa kuhakikisha angalau asilimia mbili (2%) ya maudhui yake ya siku yanahusu elimu kinyume cha Kanuni ya 23 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018; na

(c) kushindwa kuhakikisha anawasilisha kwa Mamlaka ratiba yake ya vipindi siku kumi na nne (14) kabla ya robo ya mwaka kuanza kinyume na Kanuni ya 39(4)(a) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni za Mwaka 2018.

**3.0. KUSIKILIZWA KWA UTETEZI**

Mtoa Huduma aliwasilisha utetezi wake wa kimaandishi na kufika ofisi za TCRA, Makao Makuu Dar es Salaam tarehe 24 Januari, 2025 saa tano (5:00) asubuhi akiwakilishwa na Meneja wa Kituo cha Redio Ndugu Wilfred Chilimba. Pamoja na utetezi wa maandishi, mwakilishi huyo aliwasilisha kama ifuatavyo:

**3.1** Kuhusu kubadili umiliki wa hisa pasipo idhini ya Mamlaka kinyume na Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018, Mtoa Huduma aliwasilisha kuwa, mwaka 2022 Kampuni ilipata changamoto ya kifedha ambapo ilikuwa ikishindwa kutekeleza majukumu yake ya kimsingi ikiwemo kulipa ada za leseni. Kufuatia changamoto hizo, bodi ya Wakurugenzi ya Mtoa Huduma walikaa kikao tarehe 26 Marchi 2022 na kuridhia kupoteza(*forfeit*) hisa zote za wanahisa wa awali ambao ni Bwana Castory Carlos Ndullu, Joyce John Mashimba na Ndulu Group of Companies Limited. Bodi pia iliridhia kualika taasisi yenye uwezo wa kuchukua hisa zilizopotezwa (*forfeited shares*).

**3.2** Mtoa Huduma aliendelea kuwasilisha kuwa, baada ya kupata wawekezaji wapya tarehe 29 Agosti 2022 aliiandikia Mamlaka barua yenye kumbukumbu Na. GSM110387/KEYFM/SONG/290822 kuomba idhini ya kubadili umiliki wa hisa. Hata hivyo, alijulishwa na Mamlaka kupitia aliyekuwa Meneja wa Kanda ya Kusini kuwa maombi yake alipaswa kufanya katika mtandao kupitia mfumo wa Tanzanite Portal. Mtoa huduma aliwasilisha kuwa alilipa ada kiasi cha Dola za Kimarekeni 500 kwa ajili ya maombi hayo. Hata hivyo, pamoja na kufanya malipo hayo bado maombi yake katika mfumo yanasomeka kuwa hayajakamilika.

3.3 Alipoulizwa na Mamlaka kwa nini alifanya maombi ya kubadili umuiliki wa hisa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kabla ya kupata

idhini ya Mamlaka; Mtoa huduma aliwasilisha kuwa hakuwa na uelewa kuwa alipaswa kuanza na Mamlaka ndipo aende BRELA.

3.4 Mtoa Huduma aliulizwa na Mamlaka endapo anatambua kuwa idadi ya hisa zilizofanyiwa mabadiliko ya umiliki yanamfanya kuwa na hadhi ya kuleta maombi ya leseni upya; ambapo Mtoa Huduma alikiri kujilishwa hivyo na Meneja wa Mamlaka kanda ya Kusini, hata hivyo alidai kuwa alidhani angejulishwa rasmi kupitia mfumo wa Tanzanite Portal baada ya kufanya malipo ya dola 500, kitu ambacho hakijafanyika.

3.5 **Kuhusu** kushindwa kuhakikisha angalau asilimia mbili (2%) ya maudhui yake ya siku yanahusu elimu kinyume cha Kanuni ya 23 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018, Mtoa Huduma awali katika ushahidi wake alieleza kuwa, Radio yake ina vipindi vya habari za kijamii na taarifa ya habari ambazo zimekuwa zikigusa maeneo tajwa. Aliwasilisha kuwa kwa siku za jumatatu mpaka ijumaa, Redio yake imekuwa na vipindi kama: Bahasha *ya Jamii* saa 12:00-4:00 Asubuhi, Utabiri wa hali ya hewa kutoka Mamlaka ya hali ya hewa Taznaia, Taarifa kamili ya Habari saa 1:00, kurasa za magazeti 1:30 - 2:30, Tano za Nguvu ambapo ni habari tano kubwa za mkoa wa Ruvuma, kitaifa na kimataifa, Kimeseo ambapo msikilizaji atapiga simu na kueleza kero mtaani kwake, Mtaa kwa Mtaa saa 4:00 -7:00, Dondoo za Michezo, Darasani, Pongezi na Mapishi. Aliongeza kuwa Redio yake hurusha taarifa ya habari saa 1:00-1:10. Saa 6:00 -6.10, Dira Halisi 10:00 -10:45) na Voice of America (VOA) saa 1:30 - 20:00.

3.6 Kwa siku za jumamosi, Mtoa Huduma amekuwa na vipindi vingi vya kuelimisha jamii kama Jukwaa la Wanawake saa 10:00 -12:00 jioni, Vipindi vya Shule saa 8:00 -10:00 Jioni, Kipindi cha Watoto saa 9:00-4:00 Asubuhi na Vipindi vingine kama Bahasha ya Jamii, Mtaa kwa Mtaa na vipindi vingine vyenye maudhui ya kuelimisha jamii kwa asilimia sabini (70) kama inavyosomeka katika Mpangilio wa Vipindi wa Robo ya kwanza na ya pili, mwaka 2025.

3.7 Mtoa Huduma alieleza kuwa kwa siku ya jumapili kuna kipindi cha Gospel Miracle 3:00 -8:00 mchana, kipindi hiki kinakuwa na ibada mbalimbali zinazounganishwa toka makanisa tofauti tofauti, Muziki saa 9:00 -10:00, Habari saa 10:00 -11:00 jioni, Ibada ya Pili saa 11:00 -2:00 usiku, Kipindi cha Michezo

saa 2:00 – 03:00 usiku na kiufuatiwa na kipindi cha mahusiano saa 4:00- 7:00 usiku. Alipohojiwa na Mamlaka endapo siku za jumapili amekuwa akitekeleza Kanuni kwa kuwa na maudhui yasiyopungua 2% yanayohusu elimu; alikiri kuwa kwa siku za jumapili maudhui ya kuelimisha yamekuwa hafifu ukilinganisha na siku zingine.

3.8 Kuhusu kushindwa kuwasilisha kwa Mamlaka ratiba ya vipindi siku kumi na nne (14) kabla ya robo ya mwaka kinyume cha Kanuni ya 39(4)(a) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018, Mtoa Huduma alieleza kuwa, Amri ya Utekelezaji haikueleza ni kipindi cha muda gani ambapo Mtoa Huduma alishindwa kutekeleza jukumu hilo la kisheria, hata hivyo, alieleza kuwa tangu walipopata leseni wamekuwa wakituma mpangilio wa vipindi (*program line up*). Tarehe 16 Desemba 2024 walipakia mpangilio wao wa vipindi kwenye mfumo wa Tanzanite Portal na walishangazwa kupewa taarifa na Mamlaka kuwa Mpangilio huo wa vipindi haukuwepo kwenye mfumo hivyo watume tena, ambapo walifanya kama walivyoelekezwa.

## 4.0. UZINGATIAJI WA UTETEZI

Baada ya kupitia utetezi wa Mtoa Huduma uliowasilishwa kwa maandishi na kwa mdomo, Mamlaka imezingatia utetezi huo kama ifuatavyo:

4.1 Kuhusu kubadili umiliki wa hisa pasipo idhini ya Mamlaka kinyume na Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018**,** Mamlaka imezingatia kuwa, Mtoa huduma anakiri kubadili umiliki wa hisa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) pasipo idhini ya Mamlaka kinyume na Kanuni. Kuhusu utetezi wa Mtoa Huduma kuwa hakuwa na ufahamu juu ya matakwa ya Kanuni, Mamlaka inamkumbusha Mtoa Huduma kuwa sheria inamtaka kufahamu sheria zote, hata katika leseni aliyopewa ilikuwa na sharti la kumtaka kuzingatia sharia zote za nchi. Hivyo basi, utetezi wa kuwa hakufahamu takwa hilo la kisheria hauna mashiko.

4.2 Mamlaka inatambua jitihada za Mtoa Huduma, baada ya kufahamishwa kuwa alipaswa kuomba idhini Mamlaka, kuwa alifanya hivyo katika mfumo wa Tanzanite Portal. Hata hivyo, maombi hayo imebainika kuwa kulikuwa na makosa ya kiufundi katika mfumo na kupelekea maombi hayo kutoonekana kwa upande wa Mamlaka na hivyo kushindwa kufanyiwa kazi.

4.3 Kuhusu kushindwa kuhakikisha angalau asilimia mbili (2%) ya maudhui yake ya siku yanahusu elimu kinyume cha Kanuni ya 23 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018, Mamlaka imezingatia kuwa Mtoa Huduma amekiri pia katika utetezi wake kufanya ukiukaji wa Kanuni husika hususani katika siku za jumapili. Mamlaka inaamini kuwa, Mtoa Huduma anatambua kuwa ana jukumu la kutoa elimu kwa umma kupitia chombo chake. Ukiukaji wa Kanuni husika umekuwa na madhara kwa jamii ya kitanzania.

4.4 Kuhusu kushindwa kuhakikisha anawasilisha kwa Mamlaka ratiba yake ya vipindi siku kumi na nne (14) kabla ya robo ya mwaka kinyume cha Kanuni ya 39(4)(a) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018, Mamlaka imebaini kuwa Mtoa Huduma amekuwa na uelewa mdogo wa matumizi ya mfumo wa Tanzanite Portal na hivyo kupelekea kuwasilisha taarifa sehemu ambapo Mamlaka inashindwa kuzifikia. Hivyo, Mamlaka inamshauri Mtoa Huduma kuomba huduma elekezi pale ambapo anatumia mfumo huo ili kuepuka usumbufu na ucheleweshwaji wa taarifa anazopaswa kuwasilisha.

5.0. **UAMUZI**

Baada ya kusikiliza na kuchambua utetezi wa Mtoa Huduma, Mamlaka imejiridhisha kuwa Mtoa Huduma amekiuka:

1) Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018; kwa kubadili umiliki wa hisa pasipo idhini ya Mamlaka; na
2) Kanuni ya 23 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018 kwa kushindwa kuhakikisha angalau asilimia mbili (2%) ya maudhui yake ya siku yanahusu elimu.

**HIVYO BASI,** kwa mujibu wa kifungu cha 114 cha Sheria ya Mawasiliano na Kieloctroniki na Posta [Sura ya 306] pamoja na Kifungu cha 48 (2) na (3) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania [Sura ya 172], Mamlaka:

1) inatoa **ONYO** kwa Mtoa Huduma kwa kurusha maudhui yasiyokidhi matakwa ya sheria na kanuni; na

2) inaiamuru Green Star Media Limited kukamilisha mchakato wa kubadili umiliki wa hisa.

**ENDAPO** Mtoa Huduma ataendelea na ukiukaji wa sheria na kanuni katika kipindi cha uangalizi, Mamlaka itaendelea kuchukua hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti ikiwemo **kusimamisha au kufuta** Leseni na kunyang'anya masafa.

Amri imetolewa tarehe.........28.........ya mwezi Februari 2025.

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Fri Feb 28 23:00:40 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Amri hii imepokelewa na **Green Star Media Limited** T/A **Key FM** tarehe....13/3/2025.... mwezi Machi, 2025 na:

Jina: ....TIIOH ANDREA SOVELLA....

Cheo: ....MHARIRI....

Sahihi: ................

GREEN STAR MEDIA LTD
P.O BOX 760
SONGEA
(Muhuri wa Ofisi)

*(Amri hii imetolewa katika nakala mbili (duplicate). Tafadhali weka saini katika nakala zote mbili na ubaki na nakala yako, kisha wasilisha nakala nyingine TCRA kuthibitisha kupokea Amri hii).*